

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**  
**TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA**



S.L.P. 90397,  
Simu Nambari: (022)652409165  
Nukushi:(022) 2170963  
Barua Pepe:  
[rbckinondoni@pccb.go.tz](mailto:rbckinondoni@pccb.go.tz)  
Wavuti:www.pccb.go.tz

**TAARIFA KWA VYOMBO VYA HABARI**

---

**KINONDONI, 11/08/2020**

**OFISI YA TAKUKURU MKOA WA KINONDONI YAWAFIKISHA  
MAHAKAMANI WATUHUMIWA WATATU KWA MAKOSA YA  
RUSHWA.**

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Kinondoni inatarajia kumfikisha mahakamani leo tarehe 11/08/2020 Bi. Rahma Edward Tagalile ambaye ni Afisa Mtendaji wa Mtaa wa Ada Estate kwa makosa matatu. Bi Rahman Edward atafikishwa mahakamani kwa kosa la kutumia vibaya madaraka yake na kutenda kosa kinyume na kifungu cha 31 cha sheria ya kuzuia na kupambana na rushwa Namba 11 ya mwaka 2007. Wizi akiwa mtumishi wa umma kinyume na kifungu namba 258 na 270 vya sheria ya kanuni ya adhabu namba 16 iliyofanyiwa marekebisho mwaka 2002, na kuisababishia hasara serikali kinyume na kifungu aya ya 10 (1) ya jedwali la kwanza na kifungu cha 57(1) na 60 (2) cha sheria ya uhujumu uchumi sura ya 200 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2002.

Taarifa ilipatikana kutokana na ufuatiliaji wa matumizi ya pos machine katika ukusanyaji wa mapato ya manispaa ya kinondoni, kwamba afisa mtendaji wa mtaa wa ada estate **Bi Rahma Edward Tagalile** alipewa Pos machine kwa ajili ya

kukusanya mapato ya Manispaa ya Kinondoni katika mtaa wake. Aidha Pos hiyo naye alimkabidhi mkusanya mapato ambapo mkusanya mapato huyo alifanikiwa kukusanya kiasi cha milioni nane (8,000,000/=) . Mkusanyaji wa mapato alikabidhi kiasi hicho cha fedha mtendaji wa mataa Bi. Rahma Edward Tagalile na kwamba Afisa mtendaji huyo alizifanya matumizi yake binafsi.

Hata hivyo, katika kufanyia kazi taarifa hii, uchunguzi wetu wa kina ulithibitisha kwamba ni kiasi cha shilingi 18,991,672.80 kilikusanywa na mtuhumiwa kwa ajili ya ada ya taka na kwamba fedha hizo zilitumiwa na mtuhumiwa kwa matumizi yake binafsi badala ya kuingizwa kwenye akaunti ya Manispaa ya kinondoni kwa mujibu wa sheria.

Aidha, Ofisi ya TAKUKURU Mkoa wa Kinondoni inatarajia kumfikisha Mahakamani Bw Obote Joashi Etta ambaye ni Afisa masoko wa Manispaa ya Kinondoni kwa tuhuma ya kuomba na kupokea Rushwa kinyume na kifungu cha 15 cha sheria ya kuzuia na kupambana na rushwa Na. 11/2007.

Ilipokelewa taarifa kutoka kwa mtoa taarifa wetu ikimtuhumu Bw. Obote Etta, Afisa Masoko wa Manispaa ya Kinondoni kwamba anaomba Rushwa ya shilingi 200,000/= ili kiwe kishawishi cha kumfungulia fremu zake biashara ambazo awali zilifungwa kwa makosa wa kutolipa Pango la Manispaa. Baada ya kupokea taarifa hiyo uchunguzi wa awali ulifanyika ikiwa ni pamoja na kuandaa mtego wa Rushwa hiyo na kufanikiwa kumamata Afisa huyo. Uchunguzi wetu umejiridhisha kwamba Afisa biashara huyo aliomba Rushwa kiasi cha shilingi 200,000/= ili ampatie malalamikaji funguo za Fremu zake za Bishara zilizoko katika eneo la mtaa wa mikochei B.

Pia ,TAKUKURU Mkoa wa Kinondoni inatarajia kuwafikisha mahakamani **Bw. Avitus Evodius Katura**, aliyekuwa mtendaji kata ya Kawe na **Ndg. Andrew Meku Ndaalio** ambaye ni mmiliki wa kampuni ya Ganda Classic Company Ltd kwa makosa ya kutumia nyaraka kumdanganya Mwajiri kinyume na kifungu cha 22 cha sheria ya kuzuia na kupambana na rushwa namba 11 ya mwaka 2007, kugushi kinyume na kifungu cha 333, 335(a) na 337 ya kanuni ya adhabu sura ya 16 kama ilivyofanyiwa marekebisho mwaka 2002.

Avitus Evodius Katura alipokuwa Afisa mtendaji kata ya Kawe kwa tarehe tofauti kipindi cha mwezi Juni 2015, alitumia nyaraka zilizotolewa na Ganda Classic Company Ltd kwa lengo la kufanya marejesho ya fedha kiasi cha shilingi 8,000,000/= wakati akijuwa kabisa kwamba Ganda Classic Company Ltd haikufanya matengenezo yoyote ya dharura ya barabara za mitaa ya Kawe na kulipwa fedha hizo. Pia imethibitika kwamba watuhuiwa wote wawii walikula njama na kufanikisha upatikanaji wa nyaraka zenye maelezo ya uongo na kuzitumia kufanya marejesho kwa mwajiri wao ambaye ni Mkurugenzi wa manispaa ya Kinondoni. Fedha hizo zilitolewa na mkurugenzi wa Manispaa ya Kinondoni kwa ajili ya dharura ya barabara za mitaa ya kata ya Kawe.

Takukuru Mkoa wa Kinondoni inatoa wito kwa wananchi kuendelea kutoa ushirikiano wa kutoa taarifa za vitendo vya Rushwa ili zifanyiwe uchunguzi na hatimaye wahusika wa tuhuma hizo wafikishwe mahakamani. Lengo ni kuhakikisha vitendo hivyo vinapungua kwenye jamaii na kuona kwamba wanaojihusisha na vitendo vya rushwa wanachukuliwa hatua stahili kwa mujibu wa sheria.

## **KUPAMBANA NA RUSHWA NI JUKUMU LANGU**

Imetolewa na:

**E. HAZINAMWISHO**

**Kaimu Mkuu wa TAKUKURU (M)**

**Kinondoni**